

# 60. MKRISTU MIYE.

Harmonized by:  
F.B.Mallya.

Mkri stu mi - ye! ni - ko sa - la - ma, she - ta - ni we si - ni - ji - e; si -

10

mtu - mwa - o, si - ru - di nyu - ma: mkri - stu mi - ye! mkri - stu mi - ye! 1. Mkri stu mi -

19

ye! Ba - ba ni Mu - ngu, a - mri za - ke ni ta - shi - ka. Ni -

ta - ka - a, na che - o cha - ngu ni - pa - te mi - mi o - ko - ka.

2. Mkristu miye! Yesu ni ndugu,  
Siku zote, nitampenda;  
Kwani ndiye, Mkombozi wangu,  
Kwake nimetaka kwenda.

3. Mkristu miye! na mama yangu,  
Nataka kumsikiliza;  
Ndiyo kanisa yake Mungu,  
Ndiyo yenye kunifunza.

4. Mkristu miye! si wa dunia,  
Nimekataa mamboye;  
Mungu tu nitamwelekea,  
Kwani mtoto wake miye!

5. Na alama ya ubatizo;  
ya asili dhambi sina;  
yamekwisha na maapizo,  
ya kanisa nili mwana.

6. Ni msafiri wa hapa chini;  
Ukomo juu kwa Mungu;  
Nafuliza mbio njiani;  
Mkristu miye heri yangu!